**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

# MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU WA ELIMU YA MSINGI NGAZI YA CHETI

# URAIA

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2009

ISBN ………………………………………………………….

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili au kupiga chapa au kutoa kwa namna yoyote ile muhtsari huu bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Umebuniwa na kutayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania
S. L. P. 35094
Dar-es -Salaam

Simu : +255 222 773005
Fax : +255 22 774420
Baruqa pepe : director.tie@tie.go.tz
Tovuti : www.tie.go.tz

# IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Muhtasari wa Uraia Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti** wa mwaka 2009.

**Umeidhinishwa na ……………………………………….**
**Saini ………………………………………………………**
**Tarehe ………………………………………………. 2009**
**Kamishna wa Elimu**
**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**
**S.L.P. 9121**
**DAR –ES- SALAAM**

**Simu: +255 22 2110150, 21101799, 2211046**
**Nukushi: + 255 222 11 3271**
**Tovuti: www.moe.go.tz**

## YALIYOMO


Utangulizi ..... v
Maelezo ya awali kuhusu Muhtasari huu. ..... v
Sababu za kuandaa Muhtasari huu ..... v
Madhumuni ya kufundisha somo la Uraia Ualimu ngazi ya cheti ..... vi
Muda wa Mafunzo ..... vii
Upimaji ..... viii
Mazoezi ya kufundisha kwa muda mrefu (BTP) ..... ix
1.0 DOLA ..... 1
1.1 Uraia ..... 1
1.2 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. ..... 2
1.3 Bunge na Baraza la Wawakilishi Zanzibar ..... 3
1.4 Mahakama ..... 4
1.5 Serikali/Nguzo ya Utendaji ..... 4
1.6 Serikali za Mitaa ..... 5
1.7 Utawala wa Kidemokrasia ..... 6
2.0 UTAMADUNI WETU ..... 8
2.1 Nyanja za Utamaduni ..... 8
2.2 Masuala kuhusu maisha ya familia ..... 9
2.3 Maadili ..... 10
2.4 Kazi ..... 10
2.5 Utamaduni wa Kigeni ..... 11
3.0 UCHUMI WA TANZANIA ..... 13
3.1 Nyanja za Uchumi ..... 13
3.2 Mambo yanayochangia kukua au kuporomoka kwa uchumi. ..... 14
3.2 Uchumi wa Soko Huria ..... 14
4.0 UHUSIANO WA KIMATAIFA ..... 16
4.1 Misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine. ..... 16
4.2 Maeneo ya Mahusiano ya Kimataifa. ..... 17
4.3 Utandawazi ..... 17
1.0 MISINGI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA URAIA ..... 20
1.1 Ufundishaji unaozingatia ujenzi wa stadi na ujuzi wa kiraia. ..... 20
1.2 Uchanganuzi wa masuala chanya na hasi ya serikali/siasa. ..... 21
1.3 Uhusishi wa dhana tata na uzoefu wa mwanafunzi. ..... 22
1.4 Uhusishi wa mada za Uraia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ..... 23
2.0 UCHAMBUZI WA MAANDIKO/MACHAPISHO MUHIMU YA KUFUNDISHIA /KUJIFUNZIA SOMO LA URAIA ..... 24
2.1 Uchambuzi wa Muhtasari ..... 24
2.2 Uchambuzi wa kitabu cha kiada ..... 24
2.3 Uchambuzi wa machapisho ya ziada ..... 25
2.4 Uchambuzi wa Kiongozi cha Mwalimu ..... 26
3.0 ZANA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA ..... 27
3.1 Aina za Zana ..... 27
3.2 Upatikanaji wa Zana ..... 27
3.3 Matumizi na utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia ..... 28

4.0 MAANDALIZI YA KUFUNDISHA SOMO LA URAIA ..... 30
4.1 Kuandaa maazimio ya kazi ..... 30
4.2 Kuandaa andalio la somo ..... 30
4.3 Kuandaa nukuu za somo na shajala ..... 31
5.0 UPIMAJI NA TATHMINI ..... 33
5.1 Dhana ya upimaji katika somo la Uraia. ..... 33
5.2 Zana za Upimaji katika somo la Uraia. ..... 34
5.3 Tathmini katika somo la Uraia. ..... 34
5.4 Maandalizi ya Ufundishaji wa Muda Mrefu ..... 35
REJEA ZILIZOTUMIKA ..... 37

## Utangulizi

### Maelezo ya awali kuhusu Muhtasari huu.

Muhtasari huu wa Somo la Uraia Ngazi ya Cheti umeandaliwa kuchukua nafasi ya muhtasari wa Uraia wa 1997 pamoja na muhtasari wa Mbinu za Kufundishia Maarifa ya Jamii ngazi ya cheti wa mwaka wa 2000.

Awali somo la Uraia lilianzishwa na kufundishwa kama taaluma ili kukuza na kuimarisha maarifa ya mwalimu yanayohusu jamii, uchumi, siasa na utamaduni katika taifa lake. Aidha somo la Mbinu za Kufundisha Maarifa ya Jamii lilifundishwa ili kumpatia mwalimu tarajali stadi na ujuzi wa kufundisha somo la Maarifa ya Jamii katika shule za msingi.

### Sababu za kuandaa Muhtasari huu

Mnamo mwaka 2005 somo la Maarifa ya Jamii lilivunjwa na badala yake yakaundwa masomo ya Historia, Jiografia na Uraia. Masomo haya yameanza kufundishwa katika shule za msingi kuanzia mwaka 2006. Hatua hii imesababisha kuandaliwa kwa muhtasari huu wa Uraia pamoja na mihtasari ya Histoia na Jiografia kwa ajili ya kuandaa walimu wa kufundisha masomo haya kwenye shule za msingi.

Muhtasari huu utaanza kutumika kuanzia Julai 2009 ili kuboresha mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti.Pia utawawezesha wanachuo kupata ufahamu mpana wa maarifa, stadi na mwelekeo chanya wa kufundisha somo la Uraia. Muhtasari unaweka mkazo katika kutumia njia shirikishi za kufundishia na kujifunzia, ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya vitendo, elimu jumuishi na uchopekaji wa masuala mtambuko, katika mchakato wa ufundishaji.

Muhtasari huu pia unalenga katika kuwapatia walimu wa ngazi ya cheti maarifa kuhusu mada za Uraia zinazofundishwa katika shule za msingi na ujuzi na misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia. Aidha unalenga katika kuwapatia wanachuo ujuzi wa kuchambua muhtasari wa Uraia wa shule za msingi na vifaa vingine vya mitaala; kujiandaa katika kufundisha somo na hilo, kutathmini maendeleo ya wanafunzi.

**Madhumuni ya kufundisha somo la Uraia Ualimu ngazi ya cheti**

a) Kukuza kiwango cha maarifa cha mwanachuo na uwezo wao wa kutumia njia shirikishi na ufundishaji unaojenga maana katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia.
b) Kuwawezesha wanachuo kuthamini na kudumisha utamaduni wa kitanzania, kujenga stadi za juu za kufikiri, ujuzi wa kiraia na uwezo wa kuwajengea wanafunzi stadi na ujuzi huo huo.
c) Kuandaa wanachuo kujijengea stadi na maarifa ya kushughulikia masuala mtambuko na wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwenye somo.

**Ujuzi wa somo**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili mwanachuo aweze kuwa na uwezo wa:

a) Kuchambua vifaa muhimu vya mtaala wa Uraia.
b) Kumudu mada za somo la Uraia kitaaluma na kitaalam.
c) Kutumia utaalamu katika kuchagua, kuandaa na kutumia mbinu bora na zana za kufundishia na kujifunza somo la Uraia.
d) Kuingiza stadi za juu za kufikiri, ujuzi wa kiraia na masuala mtambuko katika ufundishaji wa somo la Uraia.
e) Kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi katika somo la Uraia.
f) Kuandaa kwa ufanisi mazimio ya kazi, maandalio ya somo na nukuu za somo kwa kufundishia somo la Uraia.
g) Kukuza maendeleo ya kihaiba, kizalendo, kiteknolojia na ubunifu katika ufundishaji wa somo la Uraia.

**Malengo ya Somo**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili mwanachuo aweze:-

a) Kupitia, kuchambua na kutumia vifaa vya mtaala wa somo la Uraia katika kuanda zana za kufundishia na kujifunzia, maazimio ya kazi, maandalio ya somo, nukuu za somo na kufundisha somo kwa ufanisi.
b) Kumudu maudhui ya mada za somo la Uraia na uchopekaji wa masuala mtambuko na stadi za juu za kufikiri.
c) Kupima, kutathmini na kutumia matokeo ya upimaji na tathmini kuwasaidia wanafunzi kuwa na maendeleo mazuri katika somo la Uraia.
d) Kufundisha kwa kuzingatia umuhimu wa kuwajengea wanafunzi kujenga sifa za uzalengo, haiba na uwezo wa kutumia teknolojia ya kisasa katika kujitafutia maarifa.

e) Kuandaa na kutumia kwa uthabiti na ufanisi maazimio ya kazi, maandalio ya somo na nukuu za somo la Uraia.

f) Kutumia kwa ufasaha lugha ya kufundishia somo la Uraia shule za msingi.

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu upo katika sehemu mbili zenye mada zifuatazo:-

a) Dola
b) Utamaduni.
c) Uchumi wa Tanzania.
d) Uhusiano wa Kimataifa.
e) Misingi ya ufundishaji wa somo la Uraia.
f) Maandiko/machapisho ya kufundishia/kujifunzia somo la Uraia.
g) Zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.
h) Maandalizi ya kufundisha somo la Uraia.
i) Upimaji na Tathmini.

Mada zinazohusu dola utamaduni, uchumi wa Tanzania na uhusiano wa kimataifa zipo katika sehemu ya Taaluma na mada za misingi ya ufundishaji, maandiko/machapisho ya kufundishia somo la Uraia, zana za kufundishia na kujifunzia, maandalizi ya kufundisha na upimaji na tathmini zipo kwenye sehemu ya Ufundishaji.

Mkufunzi wa somo anategemewa kutafuta maarifa juu ya mada mbalimbali zilizomo katika muhtasari huu kutoka vyanzo mbalimbali vikiwemo vitabu, magazeti, machapisho ya ki-elimu, mtandano , DVD, CD, VHS, intaneti na kadhalika ili kuzidi kupanua kiwango chake cha kumudu somo.

Aidha, mkufunzi wa somo anahimizwa kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia zilizopendekezwa katika muhtasari huu kabla ya kutumia nyinginezo.

**Muda wa Mafunzo**

Muda wa mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni miaka 2 chuoni. Somo la Uraia lina kipindi 1 kwa wiki na muda wa kila kipindi ni saa moja (dakika 60). Katika mwaka

wa kwanza wanachuo watasoma mihula 2. Muhula I utakuwa miezi 5, au majuma 20 muhula II utakuwa miezi 3 au majuma 12.

**Upimaji**

Mwanachuo atapimwa maendeleo yake katika taaluma na ufundishaji. Katika taaluma mwanachuo atapimwa maarifa, stadi na mielekeo aliyojenga katika kujifunza sehemu hiyo. Katika ufundishaji mwanachuo atapimwa wakati wa ufundishaji wa masomo ya mfano darasani, ufundishaji wa kipindi kimoja na mazoezi ya ufundishaji kwa muda mrefu (BTP) . Mgawanyo wa alama katika upimaji wa mwanachuo utalenga sehemu zote mbili yaani taaluma na ufundishaji. Taaluma itakuwa na asilimia 20 na ufundishaji utakuwa na asilimia 30. Mtihani wa Taifa utakuwa na asilimia 50 na utafanyika mwishoni mwa muhula wa pili wa mwaka wa pili.

Mgawanyo wa alama utakuwa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Mchanganuo wa vipengele vya upimaji wa somo la Uraia**

| **No** | **Vipengele** | **Mbinu za Upimaji** | **Mwaka 1** | | **Mwaka II** | | **Kiasi (mara ngapi)** | **Jumla (Maksi)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Muhula 1** | **Muhula II** | **Muhula I** | **Muhula II** | | |
| | **Taaluma** | 1. Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 05 |
| | | 2. Kazi binafsi za mwanachuo | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 05 |
| | | 3. Mtihani wa muhula | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 10 |
| 2 | Ufundishaji | 1. Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 05 |
| | | 2. Mazoezi ya kufundisha | - | 1 | 1 | - | 2 | 10 |
| | | 3. Uandishi wa Insha | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 05 |
| | | 4. Mtihani wa muhula | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 10 |
| | | Mtihani wa Taifa (Taaluma na Ufndishaji | | | | | 50 | 50 |

Jumla ya alama za upimaji endelevu na tamati ni 100.

***NB:*** Mbinu nyingine zaidi za upimaji zitategemea na aina za upimaji kama zilivyoonyeshwa katika mwongozo (Framework)

**Mazoezi ya kufundisha kwa muda mrefu (BTP)**

Mwanachuo atapaswa kufanya mazoezi ya kufundisha kwa muda mrefu ambapo katika mwaka wa kwanza atafanya kwa wiki 8 na mwaka wa pili wiki 8.

Maelezo ya namna ya kuendesha mazoezi haya yatatolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

.

## SEHEMU YA KWANZA: TAALUMA

### 1.0 Madhumuni ya ufundishaji wa Taaluma Katika somo la Uraia

Madhumuni ya kufundisha taaluma ya somo la Uraia ni:-

a) Kukuza uwezo wa wanachuo kumudu taaluma ya somo la Uraia na kutumia vyanzo mbalimbali kutafuta maarifa ikiwepo teknolojia ya kisasa.

b) Kukuza uelewa wa wanachuo kuhusu masuala mtambuko.

c) Kukuza stadi na mielekeo ya wanachuo ili waweze kuwa chachu katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

### 2.0 Ujuzi kutokana na ufundishaji wa taaluma ya somo la Uraia

Baada ya kusoma somo la Uraia sehemu ya taaluma mwanachuo ataonesha ujuzi ufuatao:-

a) Kuchunguza, kuchambua na kupambanua masuala mbalimbali yanayohusu demokrasia, dola, uchumi, utamaduni wetu na uhusiano wa kimataifa.

b) Kuwajibika na kufanya kazi kwa uadilifu.

c) Kufikiri kiyakinifu, kujenga na kutetea hoja, kufanya maamuzi ya busara, kubaini na kukabiliana na changamoto katika maisha.

d) Mielekeo ya kuwa raia mwema mwenye kujali, kuthamini na kuheshimu haki, sheria na kanuni za nchi.

e) Kumudu maudhui ya mada za somo la Uraia katika shule za msingi.

f) Kutambua, kujadili na kufikia maamuzi sahihi kuhusu masuala mtambuko.

### 3.0 Malengo ya kufundisha ya somo la Uraia

a) Kukuza stadi za kutafuta, kuchunguza, kuchambua na kuzungumzia mambo yanayohusu masuala ya demokrasia, dola, uchumi, utamaduni wetu na uhusiano wa kimataifa.

b) Kukuza tabia ya uwajibikaji na uadilifu katika kazi na jamii.

c) Kujenga maarifa, stadi na mielekeo ya kuwa raia wenye uwezo wa kufikiri kiyakinifu, kujenga na kutetea hoja na kuchukua msimamo sahihi katika masuala ya jamii.

d) Kujenga uwezo wa kubaini na kukabiliana na changamoto mbalimbali za kisiasa, kiuchumi, kijamii na masuala mtambuko.

## SEHEMU YA KWANZA: TAALUMA

## 1.0 DOLA

### 1.1 Uraia

**Muda: Saa $5^1/_2$**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya raia na dola.
b) Kutofautisha raia na somo la Uraia.
c) Kubainisha aina na sifa za Uraia.
d) Kueleza umuhimu wa somo la Uraia.
e) Kujadili umuhimu wa haki na wajibu wa raia katika dola.

**Mbinu za kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo kupata maana ya Uraia na maana ya dola
b) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji.
c) Kusoma vitabu, tovuti husika na kuhojiana na watu mbalimbali kisha kuendesha mdahalo kuhusu umuhimu wa haki na wajibu.

**Zana za Kufundishia na kujifunzia**

a) Moduli ya somo la Uraia Ualimu Ngazi ya Cheti.
b) Chati iliyoandikwa kwa breili kuonyesha tofauti za raia na somo la Uraia.
c) Matini za aina na sifa za raia, haki na wajibu.
d) Chati inayoonesha tofauti za Uraia na somo la Uraia.
e) Vitabu vya ziada vyenye mada za Uraia na dola.
f) Makala ya sheria/sera ya Uraia.
g) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kipengele cha haki na wajibu wa raia.
h) Tovuti zinazohusu haki na wajibu wa raia.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo juu ya maana ya dola, raia na tofauti kati ya raia na somo la Uraia.

b) Maswali ya kuandika insha.

c) Taarifa kutoka kwenye tovuti.

## 1.2 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Muda: saa 5 $^{1}/_{2}$**

**Malengo mahsusi.**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha aina za katiba na sifa zake.

b) Kueleza muundo wa Katiba ya Tanzania.

c) Kujadili umuhimu wa Katiba ya Tanzania.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali vya habari, kama vile maktaba na mtandao wa intaneti.

b) Majadiliano ya vikundi.

c) Kazi za vikundi.

d) Majadiliano ya darasa.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Moduli ya somo la Uraia Ualimu Ngazi ya Cheti.

b) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c) Chati inayoonesha muundo wa Katiba ya Jamhuri Muungano wa Tanzania.

d) Mtandao wa intaneti.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo

b) Maswali ya kuandika insha

c) Maswali ya mazoezi ya kuandika.

d) Taarifa kutoka maktaba.

### 1.3 Bunge na Baraza la Wawakilishi Zanzibar

**Muda: Saa 5 ½**

**Malengo mahsusi.**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kutoafutisha Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.
b) Kueleza muundo wa Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.
c) Kuchambua shughuli za Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.
d) Kuchambua nafasi/majukumu ya chama tawala na vyama vya upinzani katika bunge, na Baraza la wawakilishi la Zanzíbar.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kusoma machapisho na kujadiliana katika vikundi.
b) Kujadiliana katika vikundi kuhusu majukumu ya chama tawala na vyama vya upinzani katika bunge.
c) Kualika mgeni.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
b) Moduli ya Uraia ngazi ya cheti.
c) Machapisho .
d) Matini zilizoandikwa kwa breili.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Maswali ya insha.
c) Kazi mradi kwa vikundi kusoma machapisho na kutafuta taarifa kutoka vyanzo.

## 1.4 Mahakama

**Muda: saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kutofautisha mfumo na muundo wa Mahakama ya Tanzania na ule wa Tanzania Zanzibar.

b) Kuainisha shughuli za Mahakama ya Tanzania na Tanzania Zanzibar.

c) Kujadili maana na umuhimu wa uhuru wa mahakama.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia.**

a) Majadiliano kwa vikundi.

b) Kusoma machapisho kwa vikundi, majadiliano ya vikundi na mawasilisho.

c) Mdahalo.

d) Majadiliano ya darasa juu ya :

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia.**

a) Moduli ya somo la Uraia, Ualimu Ngazi ya Cheti.

b) Machapisho yenye mada kuhusu mahakama.

c) Bango kitita lenye muundo na majukumu ya mahakama.

d) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

e) Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

f) Machapisho/maandiko yaliyoandikwa kwa breile.

g) Tovuti husika juu ya mahakama.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi

b) Maswali ya insha.

## 1.5 Serikali/Nguzo ya Utendaji

**Muda: saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza muundo wa Serikali ya Tanzania (Nguzo ya utendaji).

b) Kuainisha kazi za Nguzo ya utendaji na viongozi wakuu katika sehemu hiyo.
c) Kutofautisha na kulinganisha shughuli za Serikali ya Muungano na zile za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kutafuta machapisho.
b) Majadiliano kwa vikundi na kuwasilisha.
c) Maswali na majibu.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Moduli ya Uraia Ualimu Ngazi ya Cheti.
b) Machapisho.
c) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
d) Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
e) Matini zilizoandikwa kwa breile kuhusu.

**Upimaji**

a) Maswali ya zoezi.
b) Maswali ya insha.
c) Mdahalo.

### 1.6 Serikali za Mitaa

**Muda saa: 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza muundo na majukumu ya serikali za mitaa.
b) Kufafanua vyanzo na matumizi ya mapato ya serikali za mitaa.
c) Kujadili umuhimu wa serikali za mitaa kwa maendeleo ya jamii.
d) Kujadili umuhimu na namna ya ushiriki wa raia katika serikali za mitaa.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi
b) Maswali na majibu katika kufafanua vyanzo na matumizi ya mapato ya serikali za mitaa.
c) Majadiliano kwa vikundi.
d) Mdahalo kuhusu manufaa ya Serikali za Mitaa katika maendeleo ya jamii.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Matini za serikali za mitaa.
b) Moduli ya Uraia Ualimu Ngazi ya Cheti.
c) Matini iliyoandikwa kwa breili kwa ajili ya wasioona.
d) Chati za muundo wa serikali za mitaa.
e) Chati mguso.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Maswali ya insha juu ya:
    i. Muundo wa serikali za mitaa.
    ii. Namna na umuhimu wa ushiriki wa raia.
c) Kazi mradi kufuatilia shughuli za serikali za vitongoji, mitaa au vijiji na changamoto zake.

## 1.7 Utawala wa Kidemokrasia

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi.**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya demokrasia.
b) Kuchambua misingi ya Demokrasia.
c) Kueleza umuhimu wa mgawanyo wa madaraka katika utawala wa kidemokrasia.
d) Kubainisha vikwazo dhidi ya utawala wa kidemokrasia.
e) Kujadili umuhimu wa ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya vyama vingi.

f) Kujadili jinsi rushwa inavyoathiri utawala bora na haki za binadamu hapa Tanzania

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kusoma makala mbalimbali, kutembelea tovuti mbalimbali.
b) Mdahalo.
c) Majadiliano kwa vikundi na uwasilishaji.
d) Igizo – dhima na majadiliano ya vikundi au mdahalo kuonesha rushwa inavyofanyika katika jamii na athari za rushwa katika utawala bora.

**Zana za Kufundishia na kujifunzia**

a) Chati yenye misingi ya demokrasia
b) Moduli ya Uraia Ualimu ngazi ya cheti.
c) Matini zenye mada zinazohusu demokrasia.
d) Matini zilizoandikwa kwa breili.
e) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
f) Matini kuhusu rushwa inavyoathiri utawala bora na haki za binadamu.
g) Matini iliyoandikwa kwa breili.
h) Tovuti mbalimbali zinazohusu utawala wa Kidemokrasia.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Maswali ya insha.
c) Kazi mradi na utoaji ripoti.

## 2.0 UTAMADUNI WETU

### 2.1 Nyanja za Utamaduni

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kufasiri neno utamaduni.
b) Kuainisha nyanja mbalimbali za utamaduni.
c) Kujadili umuhimu wa kila nyanja ya utamaduni na utamaduni kwa jumla.
d) Kujadili mila na desturi zinazochangia ueneaji wa masuala kama UKIMWI na ubaguzi wa kijinsia na ukiukwaji wa haki za binadamu.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo na majadiliano ya darasa.
b) Kutumia machapisho kujadiliana katika vikundi na kuwasilisha.
c) Kutumia visa mafunzo katika majadiliano ya vikundi na kuwasilisha.
d) Majadiliano ya jopo.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Machapisho.
b) Picha, mikanda ya video tovuti mbalimbali, vitabu na majarida mbalimbali.
c) Matini yenye kisa mafunzo kuhusu mila na desturi zinazoweza kuchangia kupunguza kuenea kwa UKIMWI.
d) Matini zilizoandikwa kwa breili.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mazoezi ya kuandika.
c) Matumizi ya ushiriki katika majadiliano.

## 2.2 Masuala kuhusu maisha ya familia

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana, aina na umuhimu wa familia.
b) Kubainisha masuala ya kijinsia katika maisha ya familia.
c) Kubainisha mila na desturi zinazoathiri ustawi wa familia.
d) Kujadili athari za ukiukwaji wa haki na wajibu wa wanafamilia.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo au maswali na majibu.
b) Kisa mafunzo, majadiliano ya vikundi na mawasilisho.
c) Igizo dhima, majadiliano ya vikundi na mawasilisho kwa njia ya galari.
d) Mapitio ya machapisho mbalimbali, tovuti mbalimbai au kanda za video, mbinu ya kufikiri, kujozisha na kujadili na mawasilisho.
e) Midahalo.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Matini yenye kisa mafunzo.
b) Picha au kanda za videoau tovuti husika kuhusu aina za familia, masuala ya jinsia na haki na wajibu wa wanafamilia.
c) Moduli ya Uraia Ualimu ngazi ya Cheti.
d) Matini yenye kisa mafunzo iliyoandikwa kwa breili.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo na mazoezi ya kuandika.
b) Maswali ya insha.
c) Maswali ya insha kuhusu umuhimu wa kila mwanafamilia kutimiza wajibu wake.

## 2.3 Maadili

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana, mifano na umuhimu wa maadili.
b) Kubainisha mambo yanayosababisha na kudhihirisha uwepo wa mmomonyoko wa maadili katika jamii.
c) Kujadili athari za mmomonyoko wa maadili katika jamii.
d) Kujadili mbinu za kurekebisha na kudumisha maadili katika jamii.

**Mbinu zaKufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Mapitio ya machapisho mbalimbali yakiwemo magazeti, kujadiliana katika vikundi na kuwasilisha.
c) Majadiliano katika vikundi na mawasilisho.
d) Mgeni/mtaalam wa Tume ya Maadili au kiongozi wa dini.

**Vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Machapisho mbalimbali (vitabu, majarida)
b) Magazeti ya kila siku.
c) Kanda za video.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Maswali ya insha.
c) Maswali ya insha kueleza mambo yanayosababisha na kudhihirisha mmomonyoko wa maadili hapa Tanzania.

## 2.4 Kazi

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana, aina na umuhimu wa kazi kwa binadamu, hasa kwa jamii ya Tanzania.
b) Kujadili viashiria na umuhimu wa uwajibikaji katika kazi.
c) Kubainisha mambo yanayoathiri utendaji kazi.
d) Kufafanua umuhimu wa kila mtu kufanya kazi kwa bidii na uadilifu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Uchambuzi wa maandiko mbalimbali, kujadiliana katika vikundi na kuwasilisha.
c) Mbinu ya nini ninachofahamu, nini ninachotaka kufahamu na nini nilichojifunza (KWL).
d) Mgeni mwalikwa.

**Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Machapisho mbalimbali.
b) Moduli ya Uraia Ualimu Ngazi ya Cheti.
c) Tovuti mbalimbali.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Maswali ya insha.
c) Kazi mradi kubaini.

## 2.5 Utamaduni wa Kigeni

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kujadili mifano na athari za utamaduni wa kigeni kwa Tanzania.
b) Kueleza jinsi sayansi na teknolojia vinavyoathiri mila na desturi za Watanzania.
c) Kuonesha umuhimu wa jamii kuwa macho na utamaduni wa kigeni.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kutumia kanda za video au machapisho mbalimbali, mbinu ya changanya kete na majadiliano ya darasa.

b) Mdahalo.

**Vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Kanda za video na tovuti .

b) Magazeti, vijarida.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.

b) Maswali ya insha juu ya athari za sayansi na teknolojia kwa jamii.

## 3.0 UCHUMI WA TANZANIA

### 3.1 Nyanja za Uchumi

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana na umuhimu wa uchumi kwa Tanzania.
b) Kuchambua nyanja mbalimbali za uchumi.
c) Kujadili umuhimu wa nyanja mbalimbali za uchumi kwa uchumi wa Tanzania.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Kusoma machapisho mbalimbali katika vikundi kuchambua na kujadili matembezi ya galari.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Machapisho mbalimbali.
b) Picha mbalimbali.
c) Moduli ya somo la Uraia Ualimu Ngazi ya Cheti.
d) Matini zenye mada za uchumi
e) Matini zilizoandikwa kwa breile.
f) Tovuti mbalimbali zinazohusu uchumi.

**Upimaji**

a) Kazi mradi.
b) Maswali ya mdomo.
c) Maswali ya insha.

## 3.2 Mambo yanayochangia kukua au kuporomoka kwa uchumi.

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha mambo yanayochangia uchumi kukua au kuporomoka.
b) Kueleza umuhimu wa elimu, utaalamu, teknolojia, ujasiriamali, uongozi bora, mitaji, bidii ya kazi, njia bora za uchukuzi, masoko, amani na utulivu na afya ya watu, katika kukuza uchumi.
c) Kujadili umuhimu wa kutunza mazingira kwa uchumi endelevu.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Kutumia kadi za dhana, majadiliano katika vikundi na matembezi ya galari.
c) Mdahalo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Machapisho mbalimbali.
b) Kadi za dhana.
c) Tovuti mbalimbali za uchumi

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Maswali ya insha.

## 3.2 Uchumi wa Soko Huria

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya uchumi wa soko huria.
b) Kubainisha vigezo vya uchumi wa soko huria.
c) Kueleza nafasi ya Tanzania katika uchumi wa soko huria.
d) Kujadili athari za uchumi wa soko huria kwa Tanzania.

e) Kutoa mapendekezo ya namna ya kukwamua uchumi wa Tanzania.

**Mbinu za  za Kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo kujadili katika vikundi.

b) Kualika mtaalam au kujadili katika vikundi.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Machapisho na maandiko.

b) Ripoti na taarifa mbalimbali.

c) Moduli ya somo la Uraia Ualimu Ngazi ya Cheti.

d) Tovuti na Matini zenye mada za uchumi.

e) Machapisho yaliyoandikwa kwa breile.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.

b) Maswali ya insha.

c) Kazi mradi.

## 4.0 UHUSIANO WA KIMATAIFA

### 4.1 Misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine.

**Muda: saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya uhusiano wa Kimataifa na umuhimu wake.
b) Kujadili misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine.
c) Kubainisha athari za misingi hiyo kwa Tanzania.

**Mbinu za za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo, katika maktaba na intaneti.
b) Majadiliano katika vikundi na mawasilisho.
c) Mdahalo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Ramani ya dunia ya tawala za nchi.
b) Makala na magazeti mbalimbali.
c) Sera ya Tanzania ya ushirikiano wa kimataifa.
d) Mikataba ya ushirikiano wa kimataifa ambayo Tanzania imeriadhia.
e) Moduli ya Uraia Ualimu ngazi ya cheti, vitabu, vitini, matini na magazeti juu ya mashirika ya kimataifa.
f) Tovuti mbalimbali.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya mdomo na maswali ya insha.
b) Mkoba wa kazi.

## 4.2 Maeneo ya Mahusiano ya Kimataifa.

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza jinsi  Tanzania inavyohusiana na mataifa mengine kijamii.
b) Kubainisha nyanja za mahusiano ya kiuchumi kati ya Tanzania na mataifa mengine.
c) Kuonesha jinsi Tanzania inavyohusiana na mataifa mengine kisiasa.
d) Kutathmini ushirikiano wa Tanzania na mataifa mengine kijamii, kiuchumi na kisiasa.

**Mbinu za  za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo, kutafuta taarifa maktaba na kujadili katika vikundi.
b) Kufikiri na kushirkiana katika jozi, kutafuta taarifa katika maktaba, intaneti na kwenye magazeti na kufanya mdahalo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Ramani ya dunia ya tawala za nchi mbalimbali,
b) Sera ya mambo ya nje ya Tanzania,
c) Makala mbalimbali
d) Mikataba ya Ushirikiano wa Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia
e) Vitabu, vitini, matini na moduli za uraia.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Ripoti za kuandika juu ya masuala ya uhusiano wa kimataifa.
c) Maswali ya insha.

## 4.3 Utandawazi

**Muda saa 5 ½**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya utandawazi.
b) Kuchambua viashiria vya utandawazi.
c) Kujadili athari za utandawazi katika maendeleo ya Tanzania.
d) Kubainisha mikakati na changamoto za kukabiliana na athari za utandawazi.

**Mbinu za Kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo kuhusu dhana ya utandawazi.
b) Kutafuta taarifa maktaba, kujadili katika vikundi na kuwasilisha.
c) Mgeni/mtaalamu wa masuala ya uchumi.
d) Kufikiria na kushirikiana katika jozi.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Magazeti, majarida, vipeperushi, vitini, vitabu kuhusu utandawazi na moduli ya Uraia Ualimu ngazi ya cheti.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Maswali ya insha.
c) Maswali ya utafiti, maktaba na uandishi wa ripoti juu ya viashiria vya utandawazi.
d) Kazi mradi kuhusu.

## SEHEMU YA PILI: UFUNDISHAJI

**1.0 Madhumuni ya kufundisha sehemu ya ufundishaji**

Kuwawezesha wanachuo kukuza uwezo wa kuchambua mtaala wa somo la Uraia kusimamia darasa, kuendesha upimaji endelevu na kufanya tathmini ya maendeleo ya wanafunzi wao.

**2.0 Ujuzi wa Somo la Uraia: Ufundishaji.**

Baada ya kukamilisha sehemu hii mwanachuo ataonesha ujuzi ufuatao:-

a) Kuchambua mtaala wa somo la Uraia na kufanya maandalizi ya kufundisha.
b) Kutumia njia/mbinu shirikishi katika kufundisha maudhui ya somo, kuchopeka masuala mtambuko na kutumia mazingira ya elimu jumuishi.
c) Kutumia kwa ufanisi misingi ya kufundisha somo la Uraia katika ufundishaji wa somo.
d) Kutumia mbinu mbalimbali katika kusimamia darasa kupima na kutathmini maendeleo ya mwanafunzi.
e) Kubuni, kufaragua, kutengeneza na kutumia zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.

**3.0 Malengo ya somo la Uraia - Ufundishaji**.

Baada ya kujifunza sehemu ya njia/mbinu za ufundishaji mwanachuo aweze:-

a) Kuchambua muhtasari wa somo la Uraia, vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kufanya maandalizi stahili ya kufundisha, kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi.
b) Kufundisha somo la Uraia kwa kuchopeka masuala mtambuko na kwa kuzingatia elimu jumuishi.
c) Kutumia mbinu makusano za kufundishia na kujifunzia na misingi ya kufundisha somo la Uraia kwa ufanisi.

d) Kutumia kwa ufasaha lugha ya kufundishia na teknolojia ya kisasa kufundishia somo la Uraia.
e) Kufanya tafiti ndogo ndogo darasani na kuchukua hatua za haraka katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia.

## 1.0 MISINGI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA URAIA

### 1.1 Ufundishaji unaozingatia ujenzi wa stadi na ujuzi wa kiraia.

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza dhana ya stadi/ ujuzi wa kiraia
b) Kujadili umuhimu wa kujenga stadi na ujuzi wa kiraia.
c) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika kufundisha stadi/ujuzi wa kiraia
d) Kufanya onyesho mbinu juu ya uchopekwaji wa ujenzi wa stadi na ujuzi wa kiraia.
e) Maswali na majibu kuhusu dhana ya stadi/ujuzi wa kiraia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Kuchunguza na kubainisha stadi muhimu.
c) Usomaji bainifu wa matini, makala na machapisho mbalimbali.
d) Onyesho mbinu.
e) Mazoezi ya kuonyesha namna ya kuchopeka stadi na ujuzi.

**Zana/vifa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Uraia kwa shule za msingi darasa la III-VII (2006).
b) Magazeti, yenye makala mbalimbali za kisiasa
c) Maandiko.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya mdomo.
b) Uchunguzi makini na uandikaji ripoti.
c) Maswali ya insha.
d) Orodha ya uhakiki.

## 1.2 Uchanganuzi wa masuala chanya na hasi ya serikali/siasa.

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini masuala chanya na hasi ya serikali/siasa
b) Kufafanua umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi kuchanganua
c) masuala chanya na hasi ya serikali /siasa.
d) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kufundisha wanafunzi
e) kuchanganua masuala chanya na hasi ya serikali/siasa.
f) Kufanya mazoezi ya kuchanganua masuala ya serikali na siasa.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kubungua bongo, kufikiri na kushirikiana katika jozi na kuchanganua katika vikundi.
b) Kufanya maonyesho mbinu.
c) Majadiliano kwa vikundi.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Uraia kwa shule za msingi Darasa la III – VII (2006),
b) Matini ya somo la Uraia, vitini vya mada za Uraia na moduli za somo la Uraia.
c) Orodha ya masuala mbalimbali ya kiserikali na kisiasa.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya mdomo.
b) Kupima kwa kutumia orodha hakiki.

c) Mdahalo.

## 1.3 Uhusishi wa dhana tata na uzoefu wa mwanafunzi.

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha dhana tata zilizopo kwenye somo la Uraia.
b) Kuhusisha dhana zinazofundishwa na uzoefu wa mwanafunzi
c) Kueleza mambo tata muhimu ya kuzingatia katika kuhusisha dhana tata na uzoefu wa wanafunzi.
d) Kufanya mazoezi ya kuhusisha dhana tata na uzoefu wa wanafunzi.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kubungua bongo kufikiri na kushirikiana katika jozi na kujadili katika vikundi .
b) Kufanya onesho mbinu.
c) Majadiliano katika vikundi.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la uraia shule za Msingi.
b) Vitabu na moduli za ufundishaji wa somo la Uraia, shule za msingi.
c) Vitabu na matini mbalimbali.

**Upimaji**

a) Mazoezi na kuandika insha.
b) Mazoezi ya kuhusisha

## 1.4 Uhusishi wa mada za Uraia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Muda saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kubaini vipengele vya Katiba vyenye uhusiano na mada mbalimbali za somo Uraia.

b) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika kuhusisha Katiba na mada inayofundishwa

c) Kufanya mazoezi mbalimbali ya kuhusisha mada mbalimbali na vipengele muhimu vya Katiba.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo na majadiliano katika vikundi.

b) Majadiliano na mawasilisho.

c) Onesho mbinu.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Uraia katika shule za Msingi darasa la III – IV (2006),

b) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Upimaji**

a) Mazoezi kuandika na insha.

b) Utayarishaji wa jedwali la uhusisho wa mada za Uraia za shule msingi na vipengele vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c) Orodha hakiki.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAANDIKO/MACHAPISHO MUHIMU YA KUFUNDISHIA /KUJIFUNZIA SOMO LA URAIA

### 2.1 Uchambuzi wa Muhtasari

**Muda saa 7**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya muhtasari.

b) Kuchambua vipengele vikuu vya muhtasari wa somo la Uraia.

c) Kueleza sifa za muhtasari sanifu.

d) Kuchambua muhtasari wa somo la Uraia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu.

b) Kazi za vikundi

c) Majadiliano.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Nakala za muhtasari wa somo la Uraia kwa shule za msingi.

b) Maswali ya uchambuzi.

c) Moduli ya ufundishaji wa somo la Uraia ngazi ya cheti

**Upimaji**

a) Maswali ya uandishi.

b) Mazoezi ya kuandika.

c) Uandishi wa insha.

### 2.2 Uchambuzi wa kitabu cha kiada

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha sifa za kitabu cha kiada.

b) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada.
c) Kujadili faida na matatizo ya uwepo wa vitabu vya kiada kadhaa kwa ajili ya kufundisha somo la Uraia.
d) Kuchambua kitabu cha kiada.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi za vikundi kujadiliana.
b) Kazi za vikundi.
c) Usomaji wa matini.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Vitabu mbalimbali vilivyopitishwa kuwa vya kiada.
b) Maswali ya uchambuzi.
c) Moduli ya ufundishaji wa somo la Uraia ngazi ya cheti.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Ripoti ya uchambuzi.
c) Kuandika insha.

## 2.3 Uchambuzi wa machapisho ya ziada

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha machapisho ya ziada ya kufundishia somo la Uraia.
b) Kueleza sifa za machapisho bora ya ziada ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia
c) Kutafuta machapisho bora ya kufundisha somo la Uraia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

Kazi za mtu mmoja mmoja, kuchambua na kuwasilisha ripoti ya machapisho na vitabu vya ziada vinavyofaa.

**Zana/vifa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Machapisho mbalimbali ya elimu ya Uraia.
b) Vitabu mbalimbali vya ziada kwa somo la Uraia.
c) Maswali ya uchambuzi.

**Upimaji**

(i) Maswali ya insha.
(ii) Orodha ya machapisho na vitabu vya ziada kwa somo la Uraia.

## 2.4 Uchambuzi wa Kiongozi cha Mwalimu

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana, umuhimu na sifa za kiongozi cha mwalimu
b) Kuchambua kiongozi cha mwalimu kwa somo la Uraia.
c) Kueleza uhusiano uliopo kati ya muhtasari wa somo, kitabu cha kiada na kiongozi cha mwalimu kwa somo la Uraia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi za vikundi.
b) Kazi za vikundi.
c) Majadiliano ya darasa.

**Zana/vifa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Nakala za muhtasari, vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu.
b) Maswali ya uchambuzi na uoanishi.

**Upimaji**

Kazi binafsi, kuandika ripoti.

## 3.0 ZANA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA

### 3.1 Aina za Zana

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuainisha zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.

b) Kueleza umuhimu wa kutumia zana katika kufundishia/kujifunzia somo la Uraia.

c) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika kuchagua na kutumia zana za kufundishia na somo la Uraia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi

b) Maswali na majibu.

c) Igizo dhima.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Uraia shule za msingi.

b) Kiongozi cha mwalimu somo la Uraia shule za msingi.

c) Moduli ya ufundishaji somo la Uraia ngazi ya cheti.

d) Mwongozo wa kutengeneza zana.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.

b) Kuandika insha.

c) Kuandaa orodha ya zana za kufundishia na kujifunzia somo la uraia.

### 3.2 Upatikanaji wa Zana

**Muda saa 8**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa kutumia zana katika kufundishia somo la Uraia.
b) Kueleza mbinu za kupata zana za kufundishia/kujifunzia somo la Uraia.
c) Kuandaa zana za kufundishia somo la Uraia kwa kufaragua na kutengeneza.
d) Kufanya majaribio ya kufundisha kwa kutumia zana zilizoandaliwa.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano kwa vikundi.
b) Kuandaa na kukusanya vifaa au malighafi ya kutengenezea zana.
c) Kufaragua au kutengeneza zana.

**Zana/vifa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa Somo la Uraia shule za msingi.
b) Moduli ya ufundishaji Uraia ngazi ya cheti.
c) Mifano ya zana.
d) Vifaa vya kutengenezea na kufaragua zana.

**Upimaji**

Kazi mradi.

## 3.3 Matumizi na utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia

**Muda saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa kutumia zana sahihi na kwa usahihi kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.
b) Kutunza zana za kufundishia na kujifunzia somo.
c) Kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kutumia zana wakati wa ufundishaji na ujifunzaji somo la Uraia na njia bora za kuzihifadhi, zana
d) Kueleza namna na umuhimu wa kutunza zana.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Onyesho mbinu.

b) Majadiliano kwa vikundi.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la uraia shule za msingi.

b) Zana za kufundishia na kujifunzia.

**Upimaji**

a) Kuandika insha

b) Orodha hakiki a.

c) Mazoezi ya vitendo.

## 4.0 MAANDALIZI YA KUFUNDISHA SOMO LA URAIA

### 4.1 Kuandaa maazimio ya kazi

**Muda saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana na umuhimu wa azimio la kazi
b) Kufafanua vipengele vya azimio la kazi
c) Kuandaa mfano wa azimio la kazi kwa kutumia mihtasari wa Uraia shule za Msingi.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Majadiliano kwa vikundi na kuwasilisha
c) Kubaini vipengele vitakavyounda azimio la kazi.
d) Kazi kwa vikundi kuandaa mfano wa azimio la kazi.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Uraia shule za msingi.
b) Kiongozi cha mwalimu somo la Uraia shule za msingi.
c) Moduli ya ufundishia somo la uraia ngazi ya cheti.
d) Chati yenye muundo wa azimio la kazi.
e) Vitabu vya kiada somo la Uraia shule za msingi.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Portifolio ya azimio la kazi la miezi 3.

### 4.2 Kuandaa andalio la somo

**Muda saa: 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana na umuhimu wa andalio la somo
b) Kufafanua vipengele vya andalio la somo
c) Kuandaa mfano wa andalio la somo kwa kutumia vifaa husika.
d) Kueleza uhusiano kati ya azimio la kazi na andalio la somo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Majadiliano kwa vikundi.
c) Kazi kwa vikundi kuandaa andalio la somo.
d) Onyesho mbinu na mazoezi.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Azimio la kazi la somo la Uraia
b) Muhtasari wa Uraia shule za msingi.
c) Kiongozi cha mwalimu somo la Uraia shule za msingi.
d) Andalio la somo.
e) Moduli ya ufundishaji somo la Uraia ngazi ya cheti.
f) Vitabu vya kiada somo la Uraia shule za msingi.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Maswali ya mdomo.
c) Portifolio ya andalio la somo lililozingatia azimio la kazi.

## 4.3 Kuandaa nukuu za somo na shajala

**Muda saa: 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana na umuhimu wa nukuu za somo na shajala
b) Kufafanua mambo ya kuzingatia katika kuandaa nukuu za somo
c) Kuandaa mfano wa nukuu za somo la Uraia na shajala la kueleza namna ya kutumia vitu hivi.

.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano kwa vikundi.
b) Onyesho mbinu.
c) Kazi kwa vikundi katika kuandaa nukuu za somo na shajala ya somo.
d) Onyesho mbinu.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa Uraia shule za msingi.
b) Kiongozi cha mwalimu shule za msingi.
c) Matini mbalimbali zenye mada za Uraia.
d) Vitabu vya kiada na ziada vya Uraia shule za Msingi.
e) Shajala ya somo la Uraia.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo.
b) Mazoezi ya vitendo.
c) Mazoezi ya kutumia nukuu za somo katika hatua mbalimbali za somo.
d) Mazoezi ya vitendo kuonyesha namna ya kutumia shajala ya somo la Uraia.

## 5.0 UPIMAJI NA TATHMINI

### 5.1 Dhana ya upimaji katika somo la Uraia.

**Muda saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya upimaji katika somo la Uraia
b) Kufafanua umuhimu wa upimaji katika somo la Uraia
c) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika upimaji wa somo la Uraia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Bungua bongo
c) Kazi za vikundi kuandaa zana za upimaji wa somo la Uraia.
d) Kujadili katika vikundi.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Kiongozi cha mwalimu somo la Uraia shule za msingi.
b) Kitabu cha kiada cha somo la uraia shule za msingi.
c) Muhtasari wa somo la Uraia shule za msingi.
d) Machapisho na maandiko yahusuyo upimaji na tathmini.
e) Mifano mbalimbali ya zana za upimaji.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya kuandaa zana za upimaji.
b) Maswali ya zoezi

## 5.2 Zana za Upimaji katika somo la Uraia.

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha zana zinazokidhi upimaji wa somo la Uraia.
b) Kutunga maswali ya upimaji kwa kuzingatia jedwali la utahini.
c) Kuandaa mwongozo wa usahishaji.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kubungua bongo.
b) Onesho mbinu la kutunga maswali kwa kuzingatia jedwali la utahini.
c) Majadiliano ya darasa.
d) Kazi katika vikundi.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Mwongozo wa upimaji
b) Andalio la somo.
c) Mfano wa jedwali la utahini.

**Upimaji**

a) Maswali ya zoezi.
b) Mazoezi ya mtu mmoja mmoja kutunga maswali ya upimaji kwa kutumia jedwali la utahini.
c) Kazi ya vikundi.

## 5.3 Tathmini katika somo la Uraia.

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana na madhumuni ya tathmini katika somo la Uraia
b) Kuainisha mambo muhimu ya kuzingati wakati wa kufanya tathmini
c) Kubainisha aina za tathmini.

d) Kufafanua matumizi ya alama za mazoezi,majaribio na mitihani katika kuboresha ufundishaji wa somo la Uraia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi za vikundi.
b) Kubungua bongo.
c) Majadiliano kwa vikundi.
d) Maswali na majibu

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Chati ya nyanja za upimaji na ngazi zake.
b) Aina mbalimbali za maswali na muongozo wa usahihishaji.
c) Mwogozo wa upimaji na tathmini.
d) Kadi za maendeleo ya wanafunzi.

**Upimaji**

a) Zoezi la kutunga maswali ya mtihani na mazoezi kwa kuzingagia nyanja za upimaji na ngazi zake.
b) Zoezi la kusahihisha mitihani na mazoezi kwa kutumia mwongozo wa usahihishaji wa somo.

## 5.4 Maandalizi ya Ufundishaji wa Muda Mrefu

**Muda saa: 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maandalizi yanayotakiwa ya ufundishaji wa muda mrefu.
b) Kuandaa vifaa/zana muhimu zinazohitajika kwa ajili ya ufundishaji wa muda mrefu.
c) Kueleza umuhimu wa kuchunga mwenendo wake wakati wote atakapokuwa kwenye zoezi la ufundishaji wa muda mrefu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo juu ya maandalizi ya mipango ya ufundishaji wa muda mrefu.
b) Majadiliano juu ya upatikanaji, uandaaji, utengenezaji na ukusanyaji wa vifaa/zana muhimu zinazohitajika kutumika wakati wa mazoezi ya ufundishaji wa muda wa mrefu.
c) Majadiliano juu ya umuhimu wa kuchunga mwenendo wake na utendaji katika mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko kuhusu namna ya kujiandaa kwa mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu.
b) Maandiko kuhusu namna ya kujiandaa kwa mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu katika breili.
c) Muhtasari wa somo la Uraia kwa shule za Msingi (2006).
d) Makunzi anuai ya kutengenezea zana za kufundishia na kujifunzia.
e) Vyombo au vifaa vya kutengenezea zana za kufundishia.

**Upimaji**

a) Fomu ya kuchunguza au kuhakiki utengenezaji wa zana na ufaraguzi wa zana.
b) Mazoezi na majaribio.
c) Utayarishaji wa ripoti ya mazoezi ya ufundishaji.

## REJEA ZILIZOTUMIKA


Institute of Curriculum Development (1993). **A guide for Secondary School Teachers.** Ecoprint Ltd.

Institute of Curriculum Development (1993) **General Studies for Advanced level (Form V – Vi)** Ecopringit Ltd.

Ministry of Education and Vocational Training (2007) **Development Studies syllabus Diploma in Secondary Education.** Tanzania Institute of Education.

Ministry of Education and Vocational Training (2006) **Civics syllabus for Primary School.** Tanzania Institute of Education.

Ministry of Education and Vocational Training (2005) **Civics syllabus for Secondary Schools formI – IV.** Tanzania Institue of Education.

Tanzania Institute of Education (2008) **Framework for the review of Certificate Teacher Education Curriculum (Draft)**

Taasisi ya Elimu Tanzania (2002) **Civics manual for secondary school Teachers and College Tutors.**

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003) **Muhtasari wa Uraia, mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti,** Taasisi ya Elimu Tanzania

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003) **Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti** – mbinu za kufundishia maarifa ya Jamii. Taasisi ya Elimu Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2006) **Muhtasari wa somo la Uraia kwa shule za msingi,** Taasisi ya Elimu Tanzania.